**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

Boma Road,
S.L.P. 484,
SINGIDA,
Barua Pepe: rbcsingida@pccb.go.tz.
**TANZANIA.**

www.pccb.go.tz

---

**SINGIDA – APRILI 24, 2020**

**TAARIFA KWA UMMA**

## TAKUKURU MKOA WA SINGIDA YAWAPADISHA KIZIMBANI WALA RUSHWA 13 KWA TUHUMA MBALIMBALI ZA VITENDO VYA RUSHWA

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa TAKUKURU ni chombo chenye dhamana ya kusimamia Mapambano Dhidi ya Rushwa Nchini tukiongozwa na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

Ifuatayo ni Taarifa kwa Umma inayoonesha utendaji kazi wa TAKUKURU mkoa wa SINGIDA kwa kipindi cha Januari – Machi 2020 pamoja na mikakati tuliyojiwekea kwa kipindi cha Aprili – Juni 2020.

### 1. UCHUNGUZI

Katika Dawati la Uchunguzi - kipindi cha Januari – Machi, 2020 TAKUKURU Mkoa wa Singida tuliweza kutekeleza mambo yafuatayo.

### A. KESI

Jumla ya kesi Sita (06) zenye jumla ya watuhumiwa 13 zilifikishwa mahakamani na kufunguliwa mashauri ya jinai na kati ya kesi hizo, tatu zilitolewa hukumu na kushinda. Mchanganuo wa kesi hizo ni kama ifuatavyo:-

i. **Kesi ya Jinai Namba 01/2020** Mshitakiwa ni **SALIM MOHAMED SUNGI** Afisa Mtendaji wa Kijiji cha MISAKE kata ya MINYUGHE Wilaya ya IKUNGI ambaye aliomba rushwa ya Tshs. 50,000/= ili aweze kumsaidia mtoa taarifa (jina linahifadhiwa) kwenye mgogoro wa shamba kati yake na familia ya mlalamikaji. Mtego uliandaliwa na mtuhumiwa akakamatwa.

ii. **Kesi ya Uhujumu Uchumi Namba "ECC".01/2020** Washitakiwa **JOSEPH DAMAS KWEKA** ambaye alikuwa Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi LIGHWA – IKUNGI na **YASIN RASHID SHELUKINDO** ambaye alikuwa Mwalimu Shule ya Msingi LIGHWA ambao wanashitakiwa kwa kuuza jina la mwanafunzi aliyekuwa amefaulu elimu ya msingi katika shule hiyo.

iii. **Kesi ya Jinai Namba 02/2020** watuhumiwa ni **HAMDAN NASSORO HEMA** na **ISMAIL ABUBAKAR KISUNA** ambao ni Wakusanya ushuru wa TARURA Singida walituhumiwa kwa makosa ya kushawishi na kupokea Rushwa ya Sh. 20,000/= kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

    *Kesi hii ilihukumiwa mnamo 30/03/2020 na watuhumiwa walihukumiwa kifungo cha miezi sita jela kila mmoja au kulipa faini ya Tshs.500,000/= kila mmoja.*

iv. **Kesi ya Jinai Namba 03/2020** Mshitakiwa Bwana **MESHACK WILFRED MYEMBA** ambaye ni Afisa Msaidizi wa NIDA-SINGIDA anatuhumiwa kushawishi na kupokea Rushwa ya Tsh 15,000/= kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007, Mtuhumiwa alipokea Rushwa ili aweze kutoa upendeleo kwenye utoaji wa namba za kitambulisho cha Taifa kwa mtoa taarifa.

v. **Kesi ya Jinai Namba 04/2020** Washitakiwa **ADAMU JACOB GHWANGA** Mwenyekiti wa Kijiji cha MAMPANDO, **SELEMAN YUSUPH NKUMBI**, Mwenyekiti wa Kitongoji cha IKOKOLA, **RASHID ADAMU NTANDU** , Mzazi wa Mtuhumiwa **JUMA RASHID,ISSA HASSAN KINI**(Mzazi wa Mtuhumiwa) na **SUZAN DAMIANO NKINKI** (Mzazi wa Mtuhumiwa) walishawishi na kutoa hongo ya Tshs. 300,000/= ili watoto wao wasifikishwe polisi kwa tuhuma za ubakaji zilizokuwa zinawakabili.

    *Kesi hii ilihukumiwa mnamo 17/02/2020 na watuhumiwa walihukumiwa kulipa faini ya Tshs.1,000,000/=.*

vi. **Kesi ya Jinai Namba 40/2019** mshitakiwa ni **BWANA FADHILI LAURIAN BAHATI(**Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji cha MGUNGIA) na **SHABANI ATHUMANI SENGE**(Mhasibu wa serikali ya kijiji cha MGUNGIA) wameomba na kupokea rushwa kiasi cha Tsh 410,000/=ili wasimchukulie hatua za kisheria mlalamikaji baada ya kukutwa na kipande cha chuma kinachotumika katika bomba la mradi wa maji kijiji cha MGUNGIA.

    *Kesi hii ilihukumiwa mnamo tarehe 27/03/2020 kulipa faini ya Tshs.500,000/= kila mmoja.*

Vilevile katika kipindi husika TAKUKURU mkoa wa Singida ilifanya Operesheni maalum ya kufuatilia Vyama vya Ushirika.

Kupitia operesheni hii, Jumla ya fedha kiasi cha shs**. 48,906,938/=** zimeokolewa kutoka kwenye Vyama vya Ushirika baada ya viongozi na wanachama kurejesha fedha walizokuwa wanadaiwa na fedha nyingine zilizookolewa zilirejeshwa Halmashauri na kwa walalamikiaji waliofika ofisini.

## B. UTEKELEZAJI WA MAELEKEZO YA MHE. WAZIRI MKUU

Katika kutekeleza maelekezo ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Kassim Majaliwa Majaliwa aliyoyatoa kwa TAKUKURU tarehe 06/10/2019 Wilayani Iramba.

TAKUKURU tumefanikiwa kusimamia na kurejesha Tshs. 17,770,000/= za CHF IRAMBA ambazo zilitumika kinyume na utaratibu hivyo fedha hizo zimerejeshwa kwenye mfuko husika, pia vitasa 144 vyenye thamani ya Tshs. 9,360,000/= ambavyo vilifungwa tofauti na mkataba vimebadilishwa na kufungwa vipya. Aidha vitasa vingine 80 vilivyosalia ili kufikia 224 vinaendelea kubadilishwa hivyo kiasi cha Tshs. 14,560,000/= kitakuwa kimeokolewa kwenye zoezi hilo linalofanywa na Mhandisi Mshauri kwenye mradi wa ukarabati wa chuo cha ualimu Kinampanda kilichopo Wilayani Iramba.

## 2. UELIMISHAJI

Katika kuiwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa TAKUKURU mkoa wa Singida kupitia Dawati lake la Elimu kwa Umma hutumia mbinu mbalimbali kuwaelimisha na kuwashirikisha wanajamii wa makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na vijana wa shule za msingi, sekondari na vyuo.

Pia Ili kuwafikia na kuwaelimisha walengwa TAKUKURU inashirikiana na wadau wengine wa mapambano dhidi ya rushwa ambao ni pamoja na Taasisi za dini, mashirika ya Umma, mashirika yasiyo ya serikali, asasi za kiraia na sekta binafsi.

Elimu kwa Umma ilitolewa kwa makundi mbali mbali katika jamii na pia katika kipindi tajwa ofisi iliendelea kuelimisha umma juu ya madhara ya rushwa katika uchaguzi ambapo jumla ya mikutano ya hadhara **40** imefanyika ,semina **12** zimefanyika, kuimarisha vilabu vya wapinga rushwa **87** na vipindi vya redio **2** vimerushwa.

## 3. UZUIAJI RUSHWA

Katika kudhibiti mianya ya rushwa katika Idara mbalimbali TAKUKURU (M) Singida imefanya kazi ya kuchambua mifumo yenye mianya ya rushwa kwa kufanya uchambuzi wa mifumo kubaini mapungufu katika maeneo yafuatayo: Uchambuzi wa mfumo juu ya Mianya ya rushwa katika usimamizi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika Katika Halmashauri zote za Mkoa wa Singida, Uchambuzi wa mfumo wa usimamizi na udhibiti wa hifadhi za wanyamapori kwa Wilaya ya Manyoni na pia ulifanyika Uchambuzi wa mfumo wa usambazaji na matumizi ya dawa muhimu za Chanjo kwa Mkoa wa Singida.

Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Maazimio yaliyotolewa katika kikao cha wadau Ulifanyika kwa maeneo ya Manunuzi ya Umma Katika Halmashauri, Ukusanyaji mapato katika Halmashauri na Fedha za ruzuku katika shule za msingi (Capitation grants).

## 4. MIRADI YA MAENDELEO

TAKUKURU mkoa wa Singida ilifanya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kujenga uelewa wa pamoja kuhusu kiasi cha pesa kilichotengwa kwa ajili ya miradi ya ujenzi, ukarabati wa barabara, afya, elimu, maji n.k

Miradi hiyo ni ile iliyopo chini ya Mamlaka za Serikali za mitaa, wakala wa serikali na serikali kuu. Ufuatiliaji huu ulilenga pia kubaini uwiano kati ya matumizi ya fedha za umma na ubora wa huduma zinazotolewa,kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa utekelezaji wa bajeti, kuimarisha ufanisi na matokeo mazuri ya matumizi ya fedha za umma na kupata msingi wa kufanya udhibiti na ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti katika miradi husika.

Aidha katika kipindi cha Januari-Machi 2020 TAKUKURU (M) SINGIDA ilifanya ufuatiliaji miradi ya ujenzi wa Ukamilishaji na Ukarabati wa Maboma Mkoa wa Singida. Kwa ujumla katika miradi iliyochaguliwa na kufuatiliwa utekelezaji wake unaridhisha.

## 5. SHUGHULI ZA KIJAMII

Katika kuhakikisha kuwa watumishi wa TAKUKURU wanatoa mchango wao kwenye eneo hili tulifanikiwa kupanda miti 250 Kwenye eneo la Hospitali ya Ilongelo inayomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Singida. Licha ya kupanda miti hiyo tunaendelea kuisimamia ili kuhakikisha kuwa inastawi na inaleta manufaa chanya na kuwa eneo la kujifunzia utunzaji wa mazingira kwenye Taasisi za Umma na kwa watu binafsi.

## 6. MKAKATI WA UTENDAJI KAZI KUANZIA APRILI – JUNI, 2020

Mkakati wa utendaji kazi TAKUKURU (M) katika robo ya nne ya mwaka inayoanzia Aprili hadi Juni **2020** ni kuendelea kufanya Uchunguzi kwa taarifa zote za vitendo vya rushwa zitakazoibuliwa, kufanya uelimishaji kwa jamii kuhusu madhara ya rushwa hasa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka **2020,** ufuatiliaji wa kina katika miradi ya maji, na elimu kwa lengo la kuona uwiano wa fedha zilizotolewa na serikali na majengo yanayojengwa au manunuzi ya vifaa.

TAKUKURU (M) inazidi Kutoa rai kwa wananchi wote wa mkoa wa Singida kwa ujumla kujiepusha na vitendo vya Rushwa na kushiriki kikamilifu kutoa taarifa za vitendo vya Rushwa kwa kufika katika ofisi zetu za TAKUKURU (M) na Wilaya au kupiga simu ya dharura namba 113, kutuma ujumbe kwa njia ya sms au Kupiga nambari *113# na kufuata maelekezo. Pia kwa kutumia **TAKUKURU** APP hasa kwa rushwa za barabarani pale wanapobaini kutokea au kutaka kutokea kwa vitendo vya Rushwa na hatimaye kutoa ushirikiano kwenye uchunguzi ikiwa ni pamoja na kushiriki kutoa ushahidi Mahakamani.

**Imetolewa na:**

ADILI ELINIPENDA
**MKUU WA TAKUKURU (M)**
**SINGIDA**